## FUNZO LA 3

1. Maneno ya kwanza ambaye Mungu aliyaandika katika Kitabu chake ni yapi?
-Maneno ya kwanza ambaye Mungu ameyaandika katika kitabu chake ni “Hapo mwanzo.”

2. Kwa nini maneno ya Mungu ya kwanza ni, “Hapo mwanzo”?
-Kwa sababu Mungu anataka tujue kuwa kila kitu kina mwanzo.

3. Kabla ya mwanzo, kulikuwa na mito au ziwa?
-La.

4. Kabla ya mwanzo, kulikuwa milima au miti?
-La.

5. Kabla ya mwanzo, kulikuwa jua, mwezi au nyota?
-La.

6. Kabla ya mwanzo, kulikuwa wanyama au ndege?
-La.

7. Kabla ya mwanzo, kulikuwa dunia au anga?
-La.

8. Kabla ya mwanzo, kulikuwa wazungu au watu weusi?
-La.



9. Kabla ya mwanzo, roho zilikuwepo?
-La.

10. Ni nani pekee aliyekuwa anaishi kabla ya mwanzo?
-Mungu.

11. Kwa sababu ni Mungu pekee aliyeishi kabla ya mwanzo, ni nani aliye mkuu zaidi ya kila kitu?
-Mungu.

12. Kwa sababu ni Mungu pekee aliyeishi kabla ya mwanzo, ni nani pekee anayeweza kutueleza kuhusu mwanzo?
-Mungu.

13. Mungu aliaza lini?
-Mungu hana mwanzo.
-Mungu amekuwa hai wakati wote.
-Mungu ni wa milele.

14. Je, kuna aliyemzaa Mungu?
-La.
-Mungu ni wa milele.

15. Je Mungu alimzaa Mungu?
-La.
-Mungu ni wa milele.

16. Je, kuna aliyemtengeneza Mungu?
-La.
-Mungu ni wa milele.

17. Je, Mungu alitengeneza Mungu?
-La.
-Mungu ni wa milele.

18. Je, kulikuwepo wakati ambapo Mungu hakuwepo?
-La.
-Mungu amekuwa hai wakati wote.
-Mungu atakuwa hai wakati wote.

19. Watu wanahitaji chakula na maji ili waishi je, Mungu anahitaji nini ili aishi?
-Mungu haitaji chochote ili aishi.

20. Mungu anaishi vipi?
-Kwa nguvu zake mweneyewe.

-Unafikiri ni kwa nini Mungu haitaji kula chakula au kunywa maji?

-Kwa sababu Mungu hana mwili kama wanavyo wanadamu.

-Unafikiri ni kwa nini Mungu haitaji jua ili aone?

-Kwa sababu Mungu hana mwili kama wanavyo wanadamu.

-Unafikiri ni kwa nini Mungu haitaji dunia ili atembee ju yake?

-Kwa sababu Mungu hana mwili kama wanavyo wanadamu.



-Je, Mungu ana mwili?
-La.

-Je, Mungu ana mifupa?
-La.

-Je, Mungu ana damu?
-La.

-Mungu hana mwili, mifupa au damu.

-Kama Mungu hana mwili, mifupa au damu, basi Mungu ni nini?

-Mungu ni roho.

-Inamaanisha nini kuwa Mungu ni roho?

-Ufuatao ni mfano:

-Je, twaweza kuona upepo?
-La.

-Je, kuna upepo?
-Ndiyo.

-Kama vile huwezi kuona upepo, huwezi kumuona Mungu.

-Lakini kama vile upepo upo, ndivyo pia Mungu yupo.

-Hata kama huwezi kumuona Mungu, yuko.

-Mungu yuko wapi?

-Ni Mungu pekee anayeweza kutuambia yeye yuko wapi.

-Mungu anasema katika kitabu chake kuwa yuko kila mahali.

-Mungu anasema kuwa yuko kila mahali, wakati wote.

-Mungu yuko angani.
-Mungu yuko duniani.

-Mungu yuko katika mji wa Marekani sasa hivi.

-Pia yuko mji wa Afrika sasa hivi.
-Pia yuko Asia sasa hivi.

-Mungu yuko hapa sasa hivi.
-Mungu yuko kila maahali, wakati wote.

-Je, mtu anaweza kuua Marekani na Afrika kwa wakati mmoja?
-La.

-Kwa nini isiwezekane?

-Kwa sababu watu wana mwili.

-Kwa sababu watu wanaweza tu kuwa mahali pamoja kwa wakati mmoja.



-Mungu anaweza kuwa kila mahali wakati wowote kwa sababu yeye hana mwili.

-Mungu anaweza kuwa kila mahali wakati wowote kwa sababu yeye ni roho.

-Mungu yuko kila mahali wakati wowote.

-Ukiingia nyumbani mwako, nani yuko na wewe huko?
-Mungu.

-Ukienda shambani mwako, nani yuko na wewe huko?
-Mungu.

-Ukienda kumtembelea rafiki yako, nani yuko na wewe huko?
-Mungu.

-Mungu yuko kila mahali wakati wowote.

-Twaweza jificha wapi Mungu asituone?
-Hatuwezi jificha kwa Mungu.

-Kwa sababu Mungu yuko kila mahali wakati wowote, twaweza jificha asituone?
-La.

-Je, tukijaribu kujificha kileleni mwa mlima, Mungu hawezi tuona?
-La.
-Mungu yuko kila mahali.

-Je tukijaribu kujificha katika kona ya nyumba yetu, Mungu hawezi tuona?
-La.
-Mungu yuko kila mahali.

-Je tukijaribu kujificha msituni, Mungu hawezi tuona?
-La.
-Mungu yuko kila mahali.

-Hata tukijaribu mengi, hatuwezi kujificha kwa Mungu.

-Kwa nini?
-Kwa sababu Mungu yuko kila mahali wakati wowote.

-Kuna watu wanafikiria kuwa Mungu yuko kila mahali kwa sababu yeye hukimbia kwenda kila mahali.
-Hii si kweli.

-Kuna watu wanafikiria kuwa Mungu yuko kila mahali kwa sababu Mungu yuko na mwili mkubwa unaojaza dunia yote.
-Hii si kweli.

-Kuna watu wanafikiria kuwa Mungu yuko kila mahali kwa sababu Mungu huketi juu ya dunia.
-Hii pia si kweli.

-Kitabu cha Mungu kinasema kuwa, yeye ni roho na yuko kila mahali wakati wowote.

-Hakuna aliye kama Mungu.



-Ni Mungu tu anaweza kuwa kila mahali wakati wowote.

-Kila tuendapo Mungu yuko huko.

-Mungu anaweza kutuona kila wakati.

-Kuna Mungu wangapi?
-Kuna Mungu mmoja tu.

-Mungu anasema katika kitabu chake kuwa yeye ni mmoja.

-Mungu ni mmoja, na pia yuko kwa utatu.

-Je, hao watatu ambao ni Mungu mmoja ni nani?

-Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu.

-Mungu ni Mungu Baba.
-Mungu ni Mungu Mwana.
-Mungu ni Mungu Roho Mtakatifu.

-Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu ni Mungu sawa.

-Unavyoendelea kujifundisha zaidi kuhusu Mungu, utaelewa kuwa Mungu ni Mmoja na pia yuko kwa utatu.